



Watoto wa nta


 Southern African Folktale

 Wiehan de Jager

 Mutugi Kamundi

 2

 Kiswahili SW



Hapo zamani za kale, paliishi familia yenye furaha.

Hawakugombana hata kidogo. Watoto waliwasaidia wazazi nyumbani na shambani.





Lakini, walikatazwa kwenda karibu na moto.



Walifanya kazi zao zote usiku. Hii ni kwa sababu walikuwa wameumbwa kwa nta.



Lakini, kijana mmoja alitamani kwenda nje wakati wa mchana.



Siku moja tamaa ya kwenda nje ikazidi.
Wenzake wakamwonya asiende juani. Lakini,
hakusikia.

Aliyeyuka kwa sababu joto lilikuwa kali.





Watoto wa nta walihuzunika walipoona kaka yao akiyeyuka.



Wakapanga jambo fulani. Walichukua nta iliyoyeyuka wakatengeza ndege.



Wakamweka ndege huyo juu ya mlima mrefu.



Jua lilipochozoa asubuhi, akapeperuka akiimba kwa furaha.



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Watoto wa nta

-  Southern African Folktale
-  Wiehan de Jager
-  Mutugi Kamundi

